



Tel. +255784-537720/+255787-442659/+255782-250947, P.O.BOX 6049 MOROGORO E-Mail  
info@tist.org October 2011



*Member of Maendeleo Group*

**Usikate miti**



**Miti ni uhai**



**Utunze mazingira  
Nayo yakutunze  
Tuipande Miti kwa wingi**



Tel. +255784-537720/+255787-442659/+255782-250947, P.O.BOX 6049 MOROGORO E-Mail  
info@tist.org October 2011

### **Maendeleo Group.**

**Maendeleo group** was established in 2002.

This group started its official inoculation of planting trees in 2003 with 7 members, but now this group continues with tree planting but not as fast as in the beginning due to weather changing and lack of enough rainfall.



**Up to now this group** remains with 7 members. All members participate fully in their tree planting work although is not in a group way as is Best Practice since 2003.

**They are happy** is to see TIST continuing with its works with high speed especially when they read the HMM and see the TIST name is international.

**Planning and goals of our group** is to continue to plant more than 3000 trees starting next year.

### **Kikundi cha Maendeleo**

**Kikundi cha Maendeleo** kilianza mwaka 2002, Kikundi hiki kilianza rasmi kupanda miti mwaka 2003 kikiwa na wanachama 7 mpaka sasa kikundi hiki kinaendelea na shughuli za kilimo pamoja na kazi za upandaji miti japokuwa si kwa spiidi sana kama ilivyokuwa awali kulingana na mabadiliko ya hali ya hewa na mvua.



**Mpaka sasa kikundi hiki** kina Wanachama 7 wote wanashiriki vyema katika shughuli zao za upandaji Miti japokuwa si kwa pamoja ni katika maeneo yanayozunguka nyumba zao na mashamba, hii inatokana na wafanyakazi wa Mradi wa Tist ikiwa ni pamoja na Mafunzo mbalimbali kuhusu Njia Bora kuanzia mwaka 2003 na kuendelea hadi sasa.

**Kitu kilichotufurahisha** na kuwaastaajabisha ni pale walipoona Tist inaendelea na kazi zake tena kwa kasi haswa pale waliposoma kwenye Hmm na kuona jina la Tist linakuwa kimataifa.

**Mipango na Malengo ya kikundi chetu,** tunajipanga kuendelea kupand miti zaidi ya 3000 kuanzia mwakani maana kwetu huu ndiyo wakati unaofaa kwa mradi wa Tist na kuanzisha Vitaru.



Tel. +255784-537720/+255787-442659/+255782-250947, P.O.BOX 6049 MOROGORO E-Mail  
info@tist.org October 2011

The process of digging holes for planting trees and crops for 2012 has already started in many different areas. Many areas have been visited and people could be seen with happy facial expressions digging their holes. It was impressive to see people's enthusiasm in their preparations.

Our reporter was fortunate enough to be able to visit Mlali Bondeni and Ghumbi and share with two small groups there, Maendeleo and Tusahikamane. These groups have numerous nursery-ready planting trees. These groups mentioned are just some of the many groups.

Small group members are very happy with this work. One small group member said "it's a hard job but as a small group we can work together and use our combined power to do this work."

### **Planting Trees**

A really lasting way to ensure there is enough rainfall is through planting trees. If people will plant many trees over the few coming years this reforestation will help to provide enough rainfall, which will create many sources of water. So please keep planting trees to improve life for your village, country and the whole world so our children and future generations will be able to enjoy their lives too.

TIST would like to thank all the groups who have helped with this article and would like to say again that we are always ready to listen to everybody's ideas and to try them out as well. If any of you would like to write an article for Habari Moto Moto, the TIST office would be very happy to hear from you and to help you write the article. The HMM team would really like to hear news about what different groups are doing, what new ideas they have tried, what happened when they tried new things, etc.

### **THE TIST VALUES**

TIST Values are the foundation and heart of the TIST Program. Without them, the program and the work that all of us do will not thrive. This will help all the TIST participants have a better understanding of: Who we are, how we do things that other people can see; what we do and what we create. This is how we can contribute to the well being of our families and our communities and to sustain the TIST program;

Shughuli za uchimbaji wa mashimo kwa ajili ya upandaji wa miti na uandaji wa mashamba kwa ajili ya kilimo kufuatana na mpango wa TIST2012 umeshaanza katika sehemu mbalimbali. Maeneo mengi yameshatembelewa ni jambo la kufurahisha kwamba watu wengi wameanza kuchimba mashimo. Inatia moyo sana kuona watu wanaonyesha bidii katika maandalizi.

Wawakilishi wetu walipata bahati ya kutembelea Mlali Bondeni na Ghumbi hivyo kupata nafasi ya kuonana na vikundi viwili vya Maendeleo na Tushikamane. Vikundi hivi vimekwisha andaa Vitaru tayari kwa upandaji mara kipindi cha mvua kitakapoanza. Hivyo ni baadhi tu ya vikundi.

Wanavikundi wengi wanafurahia shughuli hii Mwanakikundi mmoja alisikika akisema kuwa "hii ni kazi ngumu lakini kwa kuwa tunashiriki pamoja kama kikundi tunafanikisha kazi hii"

### **Kwa kupanda miti.**

Njia ya kudumu ya kudhibiti mvua ya kutosha ni upandaji miti. Kama watu watapanda miti mingi kwa miaka michache ijayo misitu hii itasaidia kuleta mvua ya kutosha ambayo italetta vyanzo vingi vya maji. Hivyo tafadhali panda miti kwa kuendeleza maisha kwa ajili ya kijiji chako, nchi na dunia yako nzima na hivyo watoto wetu na vizazi vijavyo vingefurahia maisha yao vilevile.

TIST ingependa kushukuru vikundi vyote vilivyochangia jarida hili na ningependa kusema daima Tuko tayari kusikiliza mawazo ya kila mtu na kuyatoa. Kama yeyote kati yenu angependa kutoa habari kwa njia ya jarida la Habari Moto Moto, TIST ingefurahi kukusikiliza na kukusaidia katika uandishi wa habari yake. Kikosi cha HMM kinapenda sana kusikia mambo yanayofanywa na vikundi mbalimbali, mawazo mapya waliyojaribu kubuni, mambo yaliyotokea baada ya kubuni mawazo hayo n.k.

### **KANUNI ZA TIST**

Kwa kuanzia tunapenda kuwakumbusha kuhusu kanuni za TIST. Kanuni hizo ndizo msingi mkuu wa Mradi wa TIST. Bila kanuni hizo, mradi na kazi zote ambazo tunafanya hazitakuwa na mafanikio. Kanuni hizi zitasaidia wawakilishi wote wa mradi wa TIST kuelewa vema juu ya sisi ni nani, tunafanyaje mambo na watu wengine wanaona nini tunafanya, tunaunda nini. Hii ni kwa jinsi tunavyoweza kuchangia hata kwenye familia zetu na jamii na kuendeleza mradi wa TIST



Tel. +255784-537720/+255787-442659/+255782-250947, P.O.BOX 6049 MOROGORO E-Mail  
info@tist.org October 2011

#### Who We Are?

1. We are honest.
2. We are accurate.
3. We are transparent.
4. We are servants to each other.
5. We are mutually accountable to each other.

#### How We Do Things that other people can see

1. We are volunteers.
2. We do the work ourselves in small groups.
3. We develop and use best practices.
4. We use our head and hands are planted directly in the bags. Seeds that are suitable for this method We do other projects and businesses.
5. We sell carbon credits.

#### WHAT WE CREATE

1. We create Team Work - by doing things this way, we end up working like a team.
2. We create Capacity - we create organization, strength, and a system that is strong.
3. We create Enjoyment - we see results, we accomplish big things that we enjoy.
4. We create Big Results – by planting trees, conservation farming and from other projects and business that we do.
5. We create Low Administrative costs, yet we achieve big results. If there are things that are confusing or that you do not understand about the TIST Values, please ask questions so we can serve you better.

#### WHAT YOU NEED TO DO TO BE A TIST GROUP:

- Have at least 1000 trees per group per year.
- One acre of conservation farming per group member
- Transfer the GHG sequestration rights to UMET for the payment received.
- Use small group best practices and work together to develop and share with other groups in all areas of your lives.

Attend the closest Cluster to your small group each month.  
**Designed by Bernard Mkufya**

#### Sisi ni nani?

1. Sisi ni waaminifu
2. Sisi tupo makini
3. Sisi ni wawazi
4. Sisi ni wafanyakazi wa kila mmoja
5. Tukotayari kuwajibika kwa kila mmoja

#### Tunafanyaje mambo na watu wengine wanaona,

1. Sisi tuafanya kazi kwa kujitolea
2. Tunafanya kazi peke yetu ndani ya vikundi vidogo
3. Tunaendeleza na kutumia mbinu bora
4. Tunatumia akili na nguvu/juhudi zetu
5. Tunauza hewa taka

#### NINI TUNAFANYA

1. Tunapanda aina za miti itakayokaa kwa muda mrefu
2. Tunatafuta njia za kuboresha afya zetu
3. Tunatumia kilimo hai cha kutunza mashamba
4. Tunafanya miradi mbalimbali na biashara mbalimbali
5. Tunauza hewa taka

#### TUNABUNI NINI

1. Tunabuni kazi za pamoja- kwa njia hiyo tunafanya vitu mbalimbali, mwishoni tunapenda kufanya kama kundi
2. Tunabuni uwezo- Tumeunda makubaliano yenye nguvu na mfumo huu imara
3. Tunaunda kufurahia- Tukiona matokeo ya kukamilisha mambo makubwa tunafurahi
4. Tunabuni matokeo makubwa- katika upandaji miti, kilimo hai na katika miradi mingine na biashara tunazofanya.
5. Tunabuni gharama ndogo za kiutawala, lakini tunafanikisha mambo makubwa. Kama kuna vitu ambavyo hauelewi kuhusu Kanuni za TIST, tafadhari uliza ili uweze kuhudumia vizuri.

#### MAMBO UNAYOTAKIWA KUFANYA ILI KUWA KWENYE MRADI WA TIST

- Kuwa na angalau miti 1000 ya kikundi kila mwaka
- Kila mwanakikundi awe na ekari moja ya kilimo hai.
- Kujaza mikatabab ya kuhamishia haki za usafishaji wa hewa kwa malipo mliyokwisha lipwa.
- Kutumia njia bora za vikundi vidogo kwa kufanya kazi pamoja kuziendeleza na kushirikishana na vikundi vingine katika maeneo yenu mnayoiishi.

Kuhudhuria Klasta/Kituo kilichokaribu na kikundi chako kila mwezi